PIONEER MARK SERIES
JUNIOR SCHOOL - GRADE 7 - 2025
KISWAHILI

GOLDEN 1

NAME:.....SCHOOL:.....

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali

Kaka Fisi : (Akicheka kwa kejeli) Bi ndovu, mkulima hodari wa mihogo anayeheshimuka katika kanda hii, masalheri?

Bi Ndovu: (Akihema kwa uchovu, mzigo alionao unaonekana kumlemea) Aheri, lakini nina swali. Unacheka nini? Ama ndio njia yako ya kumfariji anayetoka kuchanika kwenye mpini siku mzima?

Kaka Fisi: (Anacheka Zaidi) Ati kuchanika kwa mpini? Wachapa kazi kama mimi hawana haja ya kujichosha. Wanafanya kazi kwa kutumia akili.

Bi Ndovu: (Kwa dharau) Mhhh! Heri nyinyi mabingwa wa kutumia akili. Sisi wengine inabidi tujikaze kisabuni ili tupate riziki

Kaka Fisi: (Akionyesha kushangaa) Nyinyi wengine! Wewe na kina nani? Je, huna habari kuwa rafikiyo sungura hapendi kupanda wala kuvuna ila daima ana shibe?

Bi Ndovu: (Kwa sauti ya chini) Hayo ya sungura hayanihusu ndewe wala sikio. Isitoshe unavyoona nimechoka, Shamba langu la mihogo liko umbali wa kilomita kumi na tano kutoka kwangu. Bado nina mlima wa kukwea ndipo nifike.

Kaka fisi: Haya basi niazime vipande viwili vya mihogo. Nitarejesha nitakapo vuna.

Bi Ndovi: Kaka fisi, umesahau kuwa tayari una deni langu la mihogo. Lipa hilo kwanza.

Kaka fisi : Nitalipa tu.

Bi Ndovu: Utanilipa mihogo ilhali hukuvuna? Unastahili kufanya kazi kwa bidii. Kumbuka ajizi ni nyumba ya njaa.

---

1. Bi Ndovu asifika kwa sababu gani? (1mk) _____
2. Kaka Fisi na Bi Ndovu walikutana wakati gani? (1mk)

   _____
3. Andika kisawe cha neno kukwea. (1mk)

   _____
4. Achanikaye kwa mpini hafi njaa, hii ni methali ina maana gani? (1mk) _____

   _____

Gari la kutupeleka mbugani lilipofika shuleni furaha ilijaa nyusoni zetu. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kutembelea mbuga la wanyama la Tsavo.Dereva aliendesha gari kwa kasi hadi kila mmoja wetu alishikilia roho mkononi.Safari ambayo kwa kawaida ingechukua muda wa masaa matatu ilichukua takribani ya masaa mawili.

Tulifika mbugani na tukaona wanyama mbalimbali. Simba anapotokea wanyama wengine lazima wampishe.Anapokuwa anatazama kwingine, Fisi alijaribu kubahatisha kumyemelea mmoja wa shibli hao. Ilikuwa kama namna ya kuwekelea kidole kwa stima. Simba alimvamia Fisi punde tu akawa msoga.

Ole wake Fisi! Badala ya yeye kusherekea kumla shibli, Simba alimsafirisha jongomeo. Kwa kweli mpiga ngumi ukutani huumiza mkonowe. Tulipoona hayo roho zetu zilidunda kama mpira uwanjani. Tulichangamana na watalii wengi siku hiyo. Kwa kweli watalii wanachangia pakubwa kuinua uchumi wa nchi yetu..

5. Ni kwanini msimulizi alikuwa na wasiwasi katika aya ya kwanza? (alm1)

_____

6. Kulingana na ufahamu, kikembe cha samba huitwaje? (alm1)

_____

7. Kwa nini simba alimshambulia fisi? (alm1)

_____

8. Ni nini maana ya "kusafishwa jongomeo"? (alm2)

_____

9. Kulingana na ufahamu watalii wanachangia kiasi gani kwa uchumi wa nchi?(alm 1)

_____

<u>Soma kifungu hiki kwa makini kisha ujibu maswali 6-10</u>

Huwa ni vigumu kupita katika miji mikuu nchini bila ya kuwaona watu maskini. Aghalabu watu hawa huwa wanawake na watoto wao. Kuna maskini ambao pia ni walemavu

Jambo linalosikitisha sana ni kuwa idadi ya maskini hao huongezeka kila kuchao badala ya kupungua. Kwa hivyo ingekuwa bora kila mmoja awajibike kutafuta suluhisho au kutafuta tatizo hili linatoka wapi.

Mara nyingi utapata watu wengi wakilaumu serikali basi hapo tutakuwa tumeandoa wajibu wa jamii ambapo hao maskini wanatoka kwa hali yeyote iwe ni serikali au jamii ni vizuri sote tuungane kupigana na janga hilo

Watu wa kuomba omba barabarani huwa hawajui kutafautisha mchana wala usiku kwa vile wao maisha yao ni pale pale kando ya barabara wakiitegemea wafadhili ambao pia unapata wengine wanatoa kwa roho ya huruma ilhali wengine wananung'unika.

10. Kulingana na aya ya kwanza ni kweli kusema kwamba masikini huonekana wapi? (alm1)

_____

11. Je ni nani anapaswa kulaumiwa juu ya umaskini? (alm1)

_____

12. Taja wafadhili aina mbili waliotajwa kwenye kifungu (alm2)

_____

13. Taja njia mbili zinazofa kutumika ili kupigana na janga la umaskini (alam2)

a) _____

b) _____

SEHEMU YA PILI LUGHA

Soma kifungu kifuatacho kisha ujubu maswali 14-18 (alm 5)

Chakula bora _14_____ **(kinadhaminiwa, kinathaminwa, kinatamaniwa, kinatazamiwa)** sana kila mahali. Thamana ya lishe bora inapatikana katika _15_____ **(uwezesho, uwezeshaji, uwezekano, uwezo)** wake wa kuingia mwili _16_____ **(dhidi ya, mbali na, licha ya, Zaidi ya)** athari tele. Chakula bora _17_____ **(hupiika, hulipa, hupaa, huyapa)** mwili uwezo mkuu wa kudhibiti maradhi kama utapiamlo. Dhibitisho_18_____ **(mzuri, kizuri, nzuri)** ni kula vyakula vyenye ladha kadha wa kadha.

SARUFI

Kuanzia swali la 19-28 jibu kulingana na maagizo

Akifisha sentensi hizi

19. Nitapanda miti mingi disemba baada ya sikukuu ya jamhuri (alm1)

_____

20. Aha kumbe mmejiunga na timu ya wangeleaji nchini kenya (alm2)

_____

21. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa nomino za makundi sahihi

a) Baba alinunua _____ la maembe sokoni.

b) Nilipopona, rafiki yangu alinileta _____ la maua.

c) Waliozua, mzozo, _____ la wazee liliingia kati na kutatua

22. Andika nomina mbili za kipekee katika sentensi ifuatayo

a) Ninaenda kujianda ili mwezi wa Aprili nizuru Nairobi

i) _____

ii) _____

23. Andika wingi wa nomino zifuatazo (alm2)
    i) Wembe _____
    ii) Chupa _____

24. Andika maneno mawili yenye sauti zifuatazo
a) dh i) _____
    ii) _____

b) th i) _____
    ii))_____

25. Taja nomino tatu za dhahania (alm3)
    i) _____
    ii) _____
    iii) _____

26. Unda nomino z vitenzijina kutokana na vitenzi vifatavyo
    a) lima _____
    b) soma _____

27. Kanusha sentensi: Mwalimu angefika mapema angetufundisha (alm2) _____
_____

28. Neno "milimani" liko katika ngeli gani? (alm2) _____
_____

SEHEMU YA TATU: FASIHI

29. Taja tanzu mbili kuu za fasihi (alm2)
    i) _____
    ii) _____

30. Taja tungo tatu za fasihi simulizi (alm3)
    i) _____
    ii) _____
    iii) _____